

USIMWAMSHE ALIYELALA

1. Wako wapi wenye ngúvu, wakivuma kama simba
Kilobaki ni kitovu, kuwa palipita mimba
Haikuwa kina ndovu, wamebaki na mitumba.
2. Pawa ni kama upepo, wavuma ukitoweka
Pawa ni machopocho, wayakumbuka wahaka
Pawa kweli ipo, au hayo madaraka?
3. Masikini roho yake, amegeuzwa kinyago
Kabaki rucha mateke, konde yake ina ndago
Awaogopa wenzake, kumzomea kwa zogo.
4. Piga konde moyo wako, kukataliwa fahari
Rejea kwa ndugu yako, mapenzi yake johari
Usijifanye mkoko, siku pita ushuwari.
5. Kamuwacha mara mia, hata haya hana tena
Kutwa kiguu na njia, kutafuta yasomana
Mapenzi yake pazia, huyaoni kwa kuona.
6. Ng'ombe hatowi maziwa, kila mwaka anazaa
Waganga wameemewa, kadhia imezagaa
Wanataka kumuuwa, kisirani wa mtaa.
7. Mtoto mwaka mmoja, enda mbio humshiki
Maneno yake ni jaa, akujibu hakuweki
Jina lake ni balaa, mjini hakumuweki.
8. Wamezaliwa ni pacha, wote watoto wa kike
Kuolewa wanakacha, wanauita uheke
Mifuko yao pakacha, nyendo zao ni za pweke.
9. Jina alibadilisha, kuvutia wanawake
Leo anaitwa kasha, kesho sihasha temeke
Majiani anakesha, kutafuta peke peke.
10. Mwenzangu wanishangaza, hebu nambie ulipo
Mwenzangu macho kengeza, wayasema yasowepo
Mwenzangu wamekuweza, kuninginia kipopo.

Wakatabahu

Hashil
November 2002